

FOMU YA MKATABA

1. MWAJIRI : / WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
CHUO CHA UALIMU NACHINGWEA
P.O.BOX 39 NACHINGWEA-LINDI

2. JINA LA FUNDI (mwajiriwa) : HASSAN MBUNDA

3. ENEO LA UJENZI : CHUO CHA UALIMU NACHINGWEA

4. MAELEZO YA KAZI KWA UFUPI: USUKAJI WA UMEME KATIKA JENGO LA
MADARASA MATATU

(Angalia Kiambatisho)

5. GHARAMA YA UFUNDI 480,000 TZS,

6. MUDA WA MKATABA: Siku 90

7. MASHARTI YA MALIPO: i) Hakuna Malipo ya Awali.

ii) Fundi atalipwa mara baada ya kazi kukaguliwa.

8. AINA YA MKATABA: Mkataba wa Ufundu

9. MASHARTI YA MKATABA:

- Mwajiri atatoa Vifaa vya ujenzi atakavyoelekezwa na Mhandisi Mshauri.
- Fundi atafanya kazi kwa Mujibu wa Mchanganuo wa kazi kwa umakini na uhodari wa hali ya juu wa kiufundi.
- Fundi asipofanya kazi yake vizuri, Mwajiri ana haki ya kusimamisha kazi na kulipa hasara zote zilizotokana na uzembe au makusudi.
- Fundi Mkuu atatoa maelekezo ya kazi kwa vibarua wake na atahusika moja kwa moja kwenye ujenzi kwa kutumia vibarua wake na kuwaunganisha mafundi wote aliowaajiri kuhakikisha kazi inafanya kulingana na taratibu za kiujenzi.
- Fundi Mkuu kwa wakati wote anatakiwa kuhakikisha yeye pamoja na mafundi wake wanazingatia nidhamu na tabia njema na asiajiri kabisa mtu asiyekuwa na utaalamu au ujuzi wa kutosha.
- Fundi Mkuu atahusika na vitendo vyote vinavyofanywa na mafundi wake na mtu yeyote anayefanya kazi chini ya usimamizi wake .


- Fundi Mkuu kwa wakati wote ahakikishe kuwa eneo la kazi linakuwa safi na salama na pia pindi kazi iishapo ahakikishe vifaa vyote vilivyosalia katika eneo la ujenzi kama mabaki vimewekwa sehemu husika na kuacha eneo likiwa safi na salama.

- Fundi ahakikishe anaondoa vitu vilivyofungwa ndani ya jengo kwa ungalifu bila kusababisha uaharibifu wa vitu hivyo au jengo.
- Kiasi cha asilimia 5% ya kiasi cha mkataba kitashikiliwa na Mwajiri kwa muda wa Mwezi mmoja baada ya kazi kukamilika (Retention Money) nakulipwa mara baada ya ukaguzi wa mwisho kufahyika.
- Ucheleweshaji wa Kazi:
 - Ucheleweshaji wa kazi uliosababishwa na fundi, fundi atapewa adhabu ya kulipa kiasi sawa na hasara iliotokana na ucheleweshaji huo
 - Ucheleweshaji uliosababishwa na Mwajiri, Fundi ataomba aongezewe muda wa kumalizia kazi.

NB: Mkataba huu unaweza kuvunjwa mara moja kwa mambo yafuatayo:

- Iwapo fundi Mkuu au Mafundi walioko chini yake au vibarua wake watajihusisha na wizi wa vifaa vya ujenzi au mali yoyote ya chuo cha ualimu Nachingwea.
- Iwapo Fundi Mkuu au Mafundi wake watafanya kazi bila kufuata mchoro au maelekezo ya Mhandisi Mshauri.
- Iwapo Fundi Mkuu au Mafundi wake hatazingatia taratibu za ujenzi au ubora wa kiufundi katika kazi yake.
- Ikumbukwe hiki ni chuo chenye vijana wa kike na kiume, hivyo basi Fundi mkuu ahakikishe vibarua wake wanakua na nidham mda wote, lugha za matusi, ulevi kelele, kusimama ovyo na wanachuo, kumletea mwanachuo zawadi yoyote, nakadhalika haviruhusiwi ndani ya eneo la chuo. Fundi mkuu atawajibishwa kwa kusitishwa mkataba wake.

MWAJIRI:

Saini: 
 Jina: MANUDI N. HAMISI
 Cheo: MKUU WA CHUO
 Tarehe: 05-02-2022

FUNDI MKUU:

Saini: H. Mbunda
 Jina: HASSAN MBUNDA
 Cheo: FUNDI UMEME
 Tarehe: 05-2-2022

SHAHIDI WA MWAJIRI

Saini: Oscar Magombana
 Jina: OSCAR MAGOMBANA
 Cheo: MUSTAFA
 Tarehe: 05-02-2022

SHAHIDI WA FUNDI MKUU

Saini: A. Selmani
 Jina: ABDUL SELMANI
 Cheo: FUNDI UMEME
 Tarehe: 05-2-2022